

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU**

Simu: 028 2770020

Nukushi:028 2770019

Barua pepe: ded.kishapudc@shinyanga.go.tz

Tovuti: www.kishapudc.go.tz



Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P 1288

Kishapu

TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Kishapu, Bwana Stephen Magoiga anawatangazia wananchi wote wa wilaya ya Kishapu kuwa tarehe 02/03/2017 kutakuwa na mkutano wa Baraza la madiwani kwa robo ya pili kwa mwaka 2016/2017. Hivyo kwa mujibu wa sheria ya serikali za mitaa namba 7 ya mwaka 1982, kifungu cha 67(1) na kanuni zake mkutano huo utakuwa wa wazi kwa wananchi wote kufika na kusikiliza utekelezaji wa shughuli na miradi mbalimbali ya maendeleo kwa robo hii.

Aidha mkutano huo utafanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya wilaya ya Kishapu kuanzia saa 4.00 Asubuhi, wananchi karibuni tuijenge Kishapu pamoja

Imetolewa na:

John Mlyambate

Mkuu wa Kitengo cha Habari, Mawasiliano na Uhusiano

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

Kishapu.

24/02/2017

